JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA SITA
JUNI 2023



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA




Utendaji wa shughuli za Serikali kufanyiwa tathimini

IDARA ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji, Serikali Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, ina jukumu kubwa la kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa sera, mipango, programu, miradi na mikakati mbalimbali inayotekelezwa ndani ya Serikali.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu, Mhe. Ummy Nderiananga alipofungua mkutano wa wadau wa maendeleo ambao pamoja na mambo mengine, ulijadili swala zima la tathmini na ufuatiliaji wa shughuli za Serikali pamoja na kongamsno la wiki ya Ufuatiliaji, Tathmini na mafunzo itakayofanyika mapema mwezi Septemba mwaka huu.

Mhe. Nderianaga alisema, baada ya Serikali kufanya maboresho ya Muundo wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) 2022/23, Idara hiyo mpya iliyoanzishwa, ndiyo inahusika moja kwa moja na kuandaa taarifa za utendaji wa Serikali za kila robo mwaka, nusu mwaka na taarifa za mwaka ikiwemo taarifa za utekelezaji wa miradi inayotekelezwa ndani ya Taasisi za Umma na utekelezaji wa Malengo ya kimataifa na kikanda na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika.

"Taarifa hizi, zitaonesha mwenendo na mwelekeo katika utendaji wa majukumu ya taasisi zote za Umma zikiwemo Wizara, Idara za Serikali zinazojitengemea, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa". Alisisistiza Naibu Waziri.

Aidha, Naibu Waziri aliendela kusema kuwa ,Taarifa ya mwaka ya utendaji wa Serikali itakuwa ikisomwa Bungeni kuanzia mwaka ujao wa fedha (2023/24) ili kutoa taswira halisi ya uwazi na uwajibikaji wa Taasisi zote za Serikali kwa Wananchi.

"ili kuwezesha Ofisi kupata taarifa hizi, itakuwa inafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa viashiria vya utendaji kazi na kutoa taarifa katika ngazi mbalimbali." Alifafanua

Awali, Naibu Waziri Nderiananga alisema kuwa Ofisi hiyo ipo maandalizi ya Kongamano la Pili la Wiki ya Kitaifa ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza linalotarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 12 – 15 Septemba, 2023 Mkoani Arusha, Kongamano ambalo litawaleta pamoja, wadau wa maendeleo wa ufuatiliaji na tathmini ya Utendaji kazi ili kupashana habari na kupeana uzoefu wa namna ya kusimamia utekelezaji wa mipango, programu na miradi mbalimbali na kuonesha namna inavyosaidia jamii.



KATIBU MKUU DKT. YONAZI Ahimiza watumishi kuwa na tabia ya kupima afya

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu amewakumbusha watumishi wa ofisi yake kuwa na tabia ya kupima afya zao mara kwa mara ili kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuyafikia malengo ya Serikali.

Ametoa kauli hiyo wakati akifungua kikao chake na watumishi wa ofisi hiyo kilichofanyika Jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Utumishi wa Umma Juni.

Katibu Mkuu huyo amesema upo umuhimu wa kujizoeza kupima afya hususan kwa magonjwa sugu yasiyoambukiza

yasiyoambukiza kwani yameendelea kuwa changamoto hasa kwa watu wenye umri mkubwa.

"Ni muhimu tumepata fursa ya kukumbushwa kupima afya zetu, hii ni changamoto inayotukabili, hivyo ni muhimu kuzingatia ushauri wa afya na masharti ya namna ya kuboresha masuala yanayohusu afya zetu, "alisema Dkt. Yonazi

Pamoja na hilo aliwakumbusha watumishi kuwa na tabia ya kufanya mazoezi ili kuendelea kutekeleza majukumu wakiwa wenye afya na kuwa na matokeo chanya.

Aidha aliutumia mkutano huo kuwaasa watumishi hao kuongeza ubunifu katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku huku wakizingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

"Mkutano huu ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ambayo tulianza kuiadhimisha tarehe 16 Juni, 2023 na leo ndio kilele.Wiki hii tunaitumia kutafakari namna tunavyotekeleza majukumu yetu kwa kipindi kilichopita, kujadili namna ya kutoa huduma bora kwa jamii ya Watanzania, kujifunza mbinu mpya na kuibua changamoto zinazotukabili katika kutekeleza majukumu yetu kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi,"alisisitiza

Pia aliwahimiza Watumishi kuendela kufanya kazi kwa upendo na kuheshimiana kwani kwa kufanya hivyo wataendelea kutekeleza majukumu yao kwa amani.

"Ni falsafa yangu kuona watu ninaowaongoza wanafanya kazi kwa upendo na kushirikiana, ni lazima kuhusiana na kuwa na mashirikiano mazuri, napenda kufanya kazi na watu wanaoheshimiana na wenye amani siamini kama mtu anaweza akafiri vizuri iwapo hana amani ndani"alisisitiza Dkt. Yonazi

Akitoa neno la shukrani Mwenyekiti ya TUGHE wa Ofisi ya Waziri Mkuu Bi. Numpe Mwambenja alipongeza uwepo wa mkutano huo huku akieleza kuwa ni nyenzo muhimu kwa kuongeza motisha kwa watumishi wa umma, na imeonesha kujali na kuendelea kuleta umoja kazini.



SERIKALI Yatia saini mkataba tathimini ya mazingira

Serikali imetia saini Mkataba wa kufanya Tathmini ya Athari ya Kimazingira na Kijamii kwa ajili ya Ununuzi wa Meli za Uvuvi , Kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP).

Akizungumza mara baada ya kutia saini mkataba huo Jijini Dodoma, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonaz amesema mkataba huo ,utawezesha kufanyika kwa tathmini ya athari ya mazingira pamoja na matengenezo ya meli zitakazotumika katika uvuvi wa Bahari Kuu ili kupata mazao ya bahari yatakayochangia katika uchumi wa Nchi.

Dkt. Yonaz aliendelea kusema kuwa, sambamba na tathmini hiyo pia utafanyika upembuzi yakinifu katika kuundwa kwa vyombo hivyo kazi itakayofanyika kwa muda wa siku 75 ambapo itagharimu shilingi milioni 349 huku akisisitiza umakini katika usimamizi wa utekelezaji wa kazi hiyo.

"Tanzania inazo rasilimali nyingi za majini, sasa ili kuhakikisha tunainua uchumi kupitia Uchumi wa Bluu Serikali imeona ni muhimu kutengeneza meli kubwa zitakazovua katika kina kirefu ili kupata mazao ya bahari ambapo meli nne zitatengenezwa kwa ajili ya Zanzibar na Meli tano kwa Tanzania Bara hivyo kukamilika kwake kutasaidia kuinua uchumi wa Taifa." Amesema Dkt. Yonazi.

Pia Katibu Mkuu huyo amewahimiza wadau wa uvuvi ambao ni Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na Shirika la Uvuvi la Zanzibar (ZAFICO) kushirikian ana Mkandarasi huyo kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kikamilifu huku akihimiza kila mmoja kuwajibika kwa sehemu yake kwa lengo la kupata matokeo chanya.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ushauri wa masuala ya Mazingira (TANSEQ) Bw. Lusako Raphael amebainisha kwamba lengo la kufanya tathimini hiyo ni kuhakikisha mradi hausababishi athari hasi katika mazingira na jamii.

"Mradi huu unalenga kuwezesha ununuzi wa meli pamoja na uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata samaki hivyo tunategemea kupata ushirikiano kutoka kwa wadau wote kama ZAFICO, TAFICO na Wizara ya Kilimo. Pia kuna mkakati wa kudhibiti athari za mazingira ambao ndiyo utakuwa muongozo wa utekelezaji wa mradi.' Ameeleza Mkurugenzi huyo.

Ikumbukwe kuwa AFDP ni mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi unaoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu ukifadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo



MEJA JENERALI MBUGE “Tuimarishe ushirikiano kukabili Majanga

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imesema itaendelea kuimarisha ushirikiano na sekta mbalimbali katika kukabiliana na maafa ili kuhakikisha wananchi wanaishi katika mazingira salama.

Kauli hiyo imetolewa Mkoani Singida na Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu Meja Jenerali Charles Mbuge wakati akifungua kikao kazi cha Watalam waliokutana kwa lengo la Kuhuisha na Kutafsiri Mwongozo wa Utekelezaji wa Dhana ya Afya Moja.

Meja Jenerali Mbuge amesema kumekuwa na ongezeko kubwa la mwingiliano wa binadamu, wanyama na mazingira ambao husababisha kutokea kwa magonjwa

mbalimbali yanayotoka kwa wanyama na kwenda kwa binadamu hivyo ipo haja ya kuwepo kwa ushirikiano wa sekta mbalimbali katika kujiandaa, kuzuia na kukabiliana na majanga hayo.

"Tunahuisha mwongozo huu kwa sababu ya mabadiliko ya sheria na kanuni za usimamizi wa Maafa. Mwongozo huu ni muhimu katika kurahisisha ushirikiano wa kisekta ili kujenga na kuimarisha ustahimilivu wa jamii dhidi ya milipuko ya magonjwa na dharura zingine zenye madhara kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira," Amesema Meja Jenerali Mbuge.

Ameongeza kuwa kwa mujibu wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa husisitiza yakiwemo Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Afya ya Wanyama (WOAH) na Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP) kwa pamoja husisitiza ushirikiano wa sekta mbalimbali ili kuwa na mikakati na sera za pamoja , katika kuimarisha afya ya wanadamu, wanyama na mazingira.

"Ili kutekeleza dhana ya Afya moja, ni muhimu kuwa na miongozo mbalimbali ili kurahishisha uratibu na utendaji katika ngazi zote. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru FAO ambao walianzisha mchakato wa kutengeneza mwongozo huu ambao katika kikao hiki utauhuishwa na kutafsiriwa," Ameeleza.

Aidha amebainisha kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa ina wajibu wa kuratibu utekelezaji wa dhana ya Afya Moja kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya 2004, Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya Mwaka 2022 na kanuni zake za mwaka 2022 pamoja na Mkakati wa Afya Moja 2022-2027.



GLOBAL FUND Kuendelea kuiunga mkono TANZANIA

SERIKALI imepongeza jitihada zinazofanywa na Mfuko wa Dunia katika kufadhili miradi inayotekelezwa kwenye afua za kupambana na UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu pamoja na uboreshaji wa mifumo ya utoaji wa huduma za afya nchini kwa lengo la kuendelea kuwa na huduma bora za afya.

Pongezi hizo zimetolewa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Sera na Uratibu wa Shughuli za Serikali Ofisi ya Waziri Mkuu Bw. Crispin Musiba alipotembela na kukagua utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Dunia katika mkoa wa Tabora ambapo walitembelea Hospitali ya Mkoa huu ya Kitete pamoja na kukagua utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa jengo la maabara katika Hospitali ya Mji Nzega

Bw. Musiba amesema kuwa, ufadhili wa miradi hiyo umeendelea kuleta tija kwa jamii kwa kuzingatia kuwa huduma zinapatika kwa ubora na kuwa na vifaa vinavyosaidia masuala ya kitabibu.

"Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo mratibu wa shughuli hii, hivyo tumeweza kujionea maendeleo ya miradi yote hususan namna vifaa vilivyonunuliwa, upanuzi wa maabara katika viwango vizuri ambapo tunaamini mradi utaendela kulifaa Taifa pamoja na mkoa kuendelea kutatua changamoto chache zilizo ndani ya uwezo wa mkoa,"aslisema Musiba

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Kamati ya Kitaifa inayoratibu na kusimamia fedha kutoka Mfuko wa Dunia (Global Fund) TNCM Dkt. Rachel Makunde ameseama ziara imeongeza tija na umuhimu wa kujionea namna mradi unavyotekelezwa kwa kuzingatia malengo yanayokusudiwa.

"Utekelezaji wa afua zilizochini ya Mfuko wa Dunia, zimeendelea kuzaa matunda kwa kuangalia hii ya ujenzi wa emergency department, pamoja na chumba cha maabara katika Hospitali ya Mkoa wa Tabora ya Kitete pamoja na hii ya Nzega, kazi inaenda vizuri na ujenzi wa maabara hapa Nzega inaridhisha,"

Aliongezea kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kuratibu na kusimamia kwa weledi maeneo yanayotekelezwa miradi hii ili kuendelea kutoa huduma bora za kiafya kwa wananchi wote.

Aidha alipongeza juhudi za mkoa kwa kutumia vyanzo vya mapato vya ndani katika ununuzi wa samani zilizohitajika katika Hospitali ya mkoa pamoja na chanagamoto kadhaa wanazokabiliana nazo.

"Global fund itaendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali, ninapongeza namna mkoa unavyokabili na kuboresha maeneo yaliyo na changamoto, kwa hapa Nzega jengo la maabara linaendelea vizuri lipo hatua za mwisho na lenye viwango vizuri hivyo thamani ya fedha zilizotolewa zinasadifu,"alisema Dkt. Rachel

Akizungumzia ziara hiyo Dkt. Rachel amesema,imelenga kutembelea mikoa sita ikiwemo Tabora,

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz